

Kumb. Na: NHC/DSM/DMP/333/172/AAJ

Tarehe: 24/02/2025

CRISTALVUE LIMITED,  
S.L.P 38331,  
**DAR ES SALAAM.**  
**SIMU: +255787873333**

YAH: KUKUBALIWA KUFANYA MATENGENEZO KATIKA KIWANJA NA. 1036-37/102  
APT NA. 314 MTA A WA MOROGORO/INDIA-DAR ES SALAAM.

Tafadhali rejea barua yako ya tarehe **17.02.2025** kuhusiana na somo tajwa hapo juu.

2. Napenda kukutaarifu kuwa maombi yako ya kutaka kuongezewa muda wa kufanya matengenezo kwenye nyumba uliyopangishwa kwa gharama zako mwenyewe bila kudai fidia kutoka Shirika la Nyumba la Taifa yamekubaliwa, matengenezo hayo yatahusisha;

- Kukarabati madirisha
- Kukarabati mlango wa grill
- Kuunganisha taa na vifaa vingine vya umeme
- Kufanya wiring ya umeme
- Kuweka partition za boards za ndani

3. Hakikisha kazi hizo zinafanyika vizuri na mtaalamu bila kuleta uharibifu wowote kwenye jengo hilo na usumbufu kwa wapangaji wengine. Umpewa muda wa miezi miwili kuanzia tarehe **24/02/2025** hadi **24/04/2025** kukamilisha kazi hii na **utaanza kulipa kodi kuanzia tarehe 01/05/2025**. Kabla ya matengenezo hayo, omba kibali kutoka Manispaa. Pia tunaomba utuletee nakala ya kibali hicho ofisi za **NHC-DAR ES SALAAM METROPOLITAN**.

4. Tafadhali usifanye kazi nyingine yoyote tofauti na maombi yako yaliyoainishwa hapo juu. Na kama utaenda kinyume na kibali hiki tutavunja mkataba wako wa upangaji.

Tunajenga Taifa letu.

  
Augustino Sanga  
**KAIMU MENEJA WA MKOA**